



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS TAMISEMI

HALMASHAURI YA WILAYA YA MUSOMA
(Barua Zote Zijibwe kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya)



Kumb. Na. E/4/2/35

14 Februari, 2022

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Musoma amepokea kibali cha ajira mbadala Kumb Na. FA.170/377/01/B/105 cha tarehe **24 Januari 2022** kwa ajili ya kuajiri Mtendaji wa Kijiji Daraja III nafasi moja (1), Dereva II nafasi Moja (01) .

Watanzania wote wenyе sifa wanakaribishwa kwa ajili ya kuomba nafasi zilizoidhinishwa kama ifuatavyo:

1.0 MTENDAJI WA KIJIZI III NAFASI MOJA (01)

1.1 MAJUKUMU YA KAZI

- a) Afisa Masuhuli na Mtendaji Mkuu wa Kijiji
- b) Kusimamia Ulinzi na Usalama wa Raia na mali zao, kuwa mlinzi wa Amani na msimamizi wa Utawala Bora katika Kijiji.
- c) Kuratibu na kusimamia upangaji na utekelezaji wa Mpango wa maendeleo ya kijiji
- d) Katibu wa mikutano na kamati zote za Halmashauri ya Kijiji.
- e) Kutafsiri na kusimamia sera, sheria na taratibu.
- f) Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali
- g) Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya Kitaalam katika Kijiji.
- h) Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na Nyaraka za Kijiji.
- i) Mwenyekiti wa kikao cha Wataalamu waliopo katika Kijiji
- j) Kupokea, kusikiliza na kutatua malalamiko na migogoro ya wananchi.
- k) Kusimamia utungaji wa Sheria ndogo za Kijiji na
- l) Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata.

1.2 SIFA ZA MWOMBAJI

- a) Awe Mtanzania
- b) Awe na Elimu ya Kidato cha nne au Sita
- c) Awe amehitimu mafunzo ya Astashahada (cheti) katika moja ya fani za Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo Dodoma au chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.
- d) Awe na umri wa miaka kumi na nane (18) au Zaidi na asiwe na umri unaozidi miaka arobaini na tano 45.
- e) Awe na Namba ya Utambulisho wa Uraia kutoka mamlaka ya vitambulisho vya Taifa (NIDA)

2.0 DEREVA II NAFASI MOJA (01)

2.1 MAJUKUMU YA KAZI

- a) Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari.
- b) Kupeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi.
- c) Kufanya marekebisho madogo madogo ya gari.
- d) Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali
- e) Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari
- f) Kufanya usafi wa gari na
- g) Kufanya kazi nyingine kadri atakavyoelekezwa na Msimamizi wake.

2.2 SIFA ZA MWOMABAJI

- a. Awe Mtanzania
- b. Awe na elimu ya kidato cha nne
- c. Awe na Leseni daraja E au C1 ya uendeshaji magari ambayo amefanyia kazi kwa muda usioupungua mwaka mmoja bila kusababisha ajali.
- d. Awe amehudhuria mafunzo ya uendeshaji magari (Basic driving Course) yanayotolewa na Chuo cha mafunzo ya ufundi stadi (VETA) au chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali.
- e. Waombaji wenge cheti cha majoribio ya ufundi Daraja II watafikiriwa kwanza.
- f. Awe na Namba ya Utambulisho wa Uraia kutoka mamlaka ya vitambulisho vya Taifa (NIDA)

4.0 UTARATIBU WA KUTUMA MAOMBI

- a) Maombi yote yatumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji, Halmashauri ya Wilaya ya Musoma, **S.L.P 344, MUSOMA.**
- b) Maombi yaambatanishwe na vyeti vya taaluma, cheti cha kuzaliwa na Kitambulisho cha NIDA au namba ya NIDA.
- c) **Testimonials Provisional result, Statement of Result** hati za matokeo ya kidato cha nne hazitataambulika .
- d) Waombaji wote waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe kuwa vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na mamlaka husika ya TCU na NECTA.
- e) Kila Mwombaji aambatanishe wasifu wake "**CV**"

5.0 MSHAHARA

Mshahara utalipwa kwa kuzingatia viwango vya Serikali **TGS B**

6.0 MWISHO WA KUPOKEA MAOMBI.

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **27/02/2022** Saa **9:30 Alasiri**



Msongela N. Palela
MKURUGENZI MTENDAJI
MUSOMA

